MTAALA WA UMILISI

Kenya Primary School Education

Assessment

G5

KISWAHILI LUGHAMUDA:

SAA 2

Soma kifungu kisha ujibu maswali.



Mimi ninaupenda mwili wangu. Nina kichwa, macho, pua na masikio. Aidha, nina mdomo,

mikono, tumbo na miguu. Kila sehemu inanisaidia. Kichwa kina ubogo ambao husaidia kufikiria.

Macho huona vitu vingi. Pua hunusa. Mdomo huzungumza na kula. Mikono hushika vitu. Masikio

husikia.Tumbo hupokea chakula. Ninatembea na kukimbia kwa miguu.

Ninaupenda mwili wangu. Ninautunza vizuri. Kila siku mimi hupiga mswaki, huoga na kuzichana

nywele zangu. Ninazikata kucha zangu mara kwa mara na kuvaa nguo safi zilizofuliwa kwa maji na

sabuni. Sote tutunze miili yetu. Tusipoitunza, itashambuliwa na magonjwa. Hatutaweza kusoma,

kucheza, kula wala kufanya kazi yoyote tukiugua.

Maswali

1. Kitu kinachosaidia kichwa kufikiri ni
   A. nywele B. ubongo
   C. shingo D. kofia.
2. Mtu akitaka kuhisi ladha ya kitu atatumia
   A. ulimi B. masikio
   C. pua D. miguu.
3. Nguo tunafua ilhali mwili tuna
   A. oga B. osha
   C. nawa D. safisha.